

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MAGU**  
(Barua zote zipelekwe kwa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya)

**MKOA WA MWANZA**  
Simu:- 028 – 2530002  
FaxNo.: -028 – 2530199



Sanduku la Posta 200  
**MAGU.**

Kumb.Na.MDC/S.10/69/80

01.08.2017

---

## **TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI**

**1.0.** Kwa Mujibu wa kibali cha Ajira Kumb. FA 170/359/01/25 cha tarehe 20/Julai /2017 kilichotolewa na Katibu Mkuu OR-Utumishi na Utawala Bora. Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Magu anawatangazia wananchi wote wenye sifa zilizoainishwa hapa chini kutuma maombi ya kazi katika Halmashauri ya Magu kwa kazi zifuatazo: -

### **1.1 Katibu Mahsusii III (Personal Secretary III) – Nafasi 1**

#### **Sifa za kuajiriwa moja kwa moja:-**

- i) Kuajiriwa wahitimu wa kidato cha IV waliofaulu Mafunzo ya Uhazili na kufaulu Mtihani hatua ya tatu.
- ii) Amefaulu somo la Hati Mkato ya Kiswahili /Kingereza maneno 80 kwa dakika moja.
- iii) Awe na cheti cha Uhazili (Certificate in Secretarial studies) na kuendelea.
- iv) Awe amepata Mafunzo ya Kompyuta kutoka Chuo chochote kinacho tambuliwa na Serikali na kupata cheti katika program za Windows, Microsoft Office, Internet, E-mail na Publisher.

#### **Majukumu:-**

- i) Kuchapa barua taarifa na Nyaraka za kawaida
- ii) Kusaidia kupokea wageni na kuwasaili shida zao na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa.
- iii) Kusaidia kutunza taarifa /kumbukumbu za matukio, miadi, wageni, tarehe za vikao, safari za Mkuu wake na Ratiba

- za kazi zingine zilizopangwa kutekelezwa katika Ofisi anapofanya kazi na kumuarifu Mkuu wake kwa wakati unaohitajika
- iv) Kusaidia kutafuta na kumpatia Mkuu wake majalada, nyaraka au kitu chochote kinachohitajika katika shughuli za kazi hapo Ofisini
  - v) Kusaidia kufikisha maelekezo ya Mkuu wake wa kazi kwa wasaidizi wake na pia kumwarifu kuhusu taarifa zozote anazokuwa amepewa na wasaidizi hao.
  - vi) Kusaidia kupokea majalada, kuyagawa kwa Maofisa walio katika sehemu alipo na kuyakusanya, kuyatunza na kuyarudisha sehemu zinazohusika.
  - vii) Kutekeleza kazi zozote atakazokuwa amepangiwa na msimamizi wake.

**Kiwango cha Mshahara:-**

TGS B – Tshs 390,000/= kwa mwezi

## 1.2 Mtendaji wa Kijiji - (Village Executive III) Nafasi 1

**Sifa za kuajiriwa moja kwa moja: -**

- i) Wahitimu wa kidato cha nne na kuendelea waliopata Mafunzo ya Taaluma katika fani ya Utawala, Sheria, Kilimo/Mifugo, Maendeleo ya Jamii na Mipango

**Makumu: -**

- i) Atakuwa Mtendaji Mkuu wa Kijiji na mshauri wa Serikali ya Kijiji na Kamati zake katika mipango ya Maendeleo.
- ii) Atakuwa Katibu na Mtunza kumbukumbu za vikao vyote vya Kijiji.
- iii) Atakuwa Afisa Mhasibu wa Serikalil ya Kijiji na atasimamia Mapato na Matumizi ya Serikali ya Kijiji.
- iv) Atakuwa kiongozi wa Watendaji wengine wa Kijiji.
- v) Atakuwa Mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala bora katika Kijiji.
- vi) Ataratibu na kusimamia utekelezjai wa Sheria ndogondogo za Serikali ya Kijiji.
- vii) Atasimamia upangaji wa utekelezjai wa Mipango ya Maendeleo ya Kijiji.
- viii) Atafanya kazi nyingine kama atakavyoolekezwa na Mkuu wake wa kazi.

**Kiwango cha Mshahara:**

TGS B – Tshs 390,000/= kwa mwezi

## **2.0. Masharti ya Jumla kwa waombaji:**

Waombaji wote wanatakiwa kuambatisha vitu vifuatavyo: -

- i) Barua ya maombi iliyoandalishiwa kwa mkono
- ii) Picha 2 (mbili) ndogo za hivi karibuni
- iii) Wasifu wa mwombaji (CV)
- iv) Vyeti vya kuzaliwa, shule na Taaluma – Vithibitishwe na Hakimu ama Wakili – Results Slip na Progress Report hazitakubaliwa.
- v) Awe na Umri chini ya miaka 38
- vi) Asiwe amewahi kuhukumiwa kifungo jela au kufukuzwa kazi.
- vii) Mwombaji awe tayari kufanya kazi Magu pasipo kuhama ndani ya miaka mitatu.

## **3.0. Usaili:**

Tarehe ya Usaili kwa waombaji watakaofanikiwa kufaulu kwenye mchujo (**Shortlisting**) itatangazwa. Aidha, siku ya Usaili mwombaji aje na vyeti halisi vya ELimu na Taaluma. Taarifa ya Polisi (Loss Report) kuhusiana na vyeti , Result slip havitapokelewa.

## **4.0. Ajira:**

Mwombaji atakayefanikiwa atajulishwa tarehe ya kuripoti.

Tarehe ya mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 21/8/2017 saa 9.30 Mchana.

### **Maombi yatumwe kwa:-**

Mkurugenzi Mtendaji,  
Halmashauri ya Wilaya ya Magu,  
S.L.P 200  
**MAGU.**

Imetolewa na:-

Lutengano G. Mwalwiba  
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**